Biblia inasema Nuhu alikuwa na watoto watatu tu! SHEMU, HAMU na YAFETI, ambao wote walikuwa wakiume.

> *Mwanzo 5:32 “Nuhu alikuwa mwenye miaka mia tano, Nuhu akawazaa Shemu, na Hamu, na Yafethi”*
>
> *Mwanzo 10:1 “Hivi ndivyo vizazi vya wana wa Nuhu, Shemu, na Hamu, na Yafethi. Na kwao walizaliwa wana wa kiume baada ya gharika”.*

Na Hao ndio walioingia kwenye safina pamoja na wake zao.

> *Mwanzo 7:7 “Nuhu akaingia katika safina, yeye, na wanawe, na mkewe, na wake za wanawe pamoja naye; kwa sababu ya maji ya gharika”.*

Hivyo ndani ya safina kulikuwa na watu 8 tu!

Inasikitisha kiasi gani? watu 8 tu ndio waliopona kati ya mabilioni waliokuwa wanaishi duniani?..Mlango wa safina ulipofungwa watu

walitamani kuingia lakini wakashindwa.

Na sisi je tutapataje kupona tusipouthamini wokovu mkuu namna hii? (Waebrania 2:3). Na dunia hii ya mwisho biblia inasema watakaopona ni wachache sana, watakaonyakuliwa ni wachache sana..Ni wale tu watakaojitahidi kuingia kwa kupitia mlango mwembamba

> *Luka 13.24 "Jitahidini kuingia katika mlango ulio mwembamba, kwa maana nawaambia ya kwamba wengi watataka kuingia, wasiweze.*
>
> *25 Wakati mwenye nyumba atakaposimama na kuufunga mlango, nanyi mkaanza kusimama nje na kuubisha mlango, mkisema, Ee Bwana, tufungulie; yeye atajibu na kuwaambia, Siwajui mtokako;*
>
> *26 ndipo mtakapoanza kusema, Tulikula na kunywa mbele yako, nawe ulifundisha katika njia zetu.*
>
> *27 Naye atasema, Nawaambia, Siwajui mtokako; ondokeni kwangu ninyi nyote mlio wafanyaji wa udhalimu".*

Tujitahidi tuwe mimi na wewe

Maran atha!

---

Mada Nyinginezo:

NUHU ALIJENGA SAFINA KWA MIAKA MINGAPI?[1]

NUHU ALIISHI MIAKA MINGAPI?[2]

NUHU ALIWALETAJE LETAJE WANYAMA KWENYE SAFINA?[3]

NUHU WA SASA NI YUPI?.[4]

---

Rudi Nyumbani:[5]

Share on:
WhatsApp
Endnotes:

1. NUHU ALIJENGA SAFINA KWA MIAKA MINGAPI?: https://wingulamashahidi.org/2019/10/13/nuhu-alijenga-safina-kwa-miaka-mingapi/

2. NUHU ALIISHI MIAKA MINGAPI?: https://wingulamashahidi.org/2019/10/13/nuhu-aliishi-miaka-mingapi/
3. NUHU ALIWALETAJE LETAJE WANYAMA KWENYE SAFINA?: https://wingulamashahidi.org/2019/09/02/nuhu-alipataje-ujuzi-wa-kuwatambua-wanyama-wale-wote-na-kuwaweka-ndani-ya-safina/
4. NUHU WA SASA NI YUPI?.: https://wingulamashahidi.org/2019/01/01/nuhu-wa-sasa/
5. Rudi Nyumbani:: https://wingulamashahidi.org